

Faida za udijitalishaji wa lugha

TRANSLATION
COMMONS



2022-2032 | INTERNATIONAL DECADE OF

Indigenous Languages

Faida za udijitalishaji wa lugha

Tunatumaini kwamba mfululizo wa miongozo au hatua zinazochukua lugha kutoka kutokuwepo kabisa katika mazingira ya kidijitali (sifuri) hadi kutumika kikamilifu, utatoa njia iliyo wazi kwa kila jamii ya lugha inayovutiwa kidijitali lugha yake, iwapo zitapenda kufurahia uwezo kamili wa matumizi ya kompyuta katika lugha yao ya asili.

Faida za kuifanya lugha iwe katika mfumo wa kidijitali zitategemea malengo ya jamii ya wazungumzaji wake. Malengo hayo yanaweza kujumuisha kusherehekea uzuri wa lugha, kuhifadhi mifumo ya maarifa, kusambaza maadili, kuunda programu na bidhaa, kushirikisha hadithi na historia, kuwezesha usimamizi wa mazingira na uongozi wa fikra, pamoja na kupanua biashara, elimu, ajira, burudani, afya, na usalama. Uwekaji wa lugha katika mfumo wa kidijitali huruhusu jamii kunufaika na seti inayozidi kupanuka ya zana zinazotegemea kompyuta. Zana hizi hutumika katika kuhifadhi, kufufua, na kufundisha lugha. Uwepo imara wa kidijitali mtandaoni, na hivyo kuongezeka kwa mwonekano, unaweza kusaidia kushawishi sera za serikali ili kuunga mkono jamii za asili na kuzihamasisha biashara kuelekea ujumuishaji. Kwa kuzingatia kuenea kwa matumizi ya simu janja miongoni mwa vijana, udijitalishaji unaweza kuwa njia ya asili ya kuwahusisha na lugha mama yao. Mwonekano mkubwa zaidi kupitia majukwaa ya kidijitali unaweza kusababisha fursa zaidi na ongezeko la mahitaji ya wazungumzaji wa lugha za asili.

Jamii za lugha zinapo chukua nafasi yao katika jukwaa la kimataifa kupitia majukwaa ya kidijitali, hunufaisha dunia kwa ujumla. Uzoefu wao, maarifa, na mitazamo yao ya kipekee kuhusu ulimwengu hutoa mchango muhimu kwa jamii zingine duniani, na mwingiliano unaotokana na hilo unaweza kuleta suluhu mpya kwa matatizo ya dunia. Udijitali hurahisisha uhifadhi na uchapishaji wa taarifa hizi, na hivyo kufanya upeo na asili ya lugha za binadamu vipatikane kwa dunia nzima na zihifadhiwe kwa manufaa ya ubinadamu kwa njia ambazo bado hatuwezi kuzitabiri.

Kwa kifupi baadhi ya faida zinazopatikana kutokana na kuifanya lugha iwe ya kidijitali ni:

- Kuwawezesha wazungumzaji wa lugha moja kufikia kwa urahisi, kuunda na kubadilishana maudhui katika lugha yao ya asili, ikiwemo mawasiliano ya masafa marefu na kwa watu binafsi au makundi makubwa.
- Kuongeza upatikanaji wa taarifa za matibabu na huduma za afya.
- Kusaidia mawasiliano katika dharura ya kuokoa maisha na katika majanga.
- Kupanua biashara za ndani na za mtandaoni.
- Kufungua njia mpya za kushirikiana na kusambaza sanaa, uongozi wa fikra, na falsafa.
- Kukuza nyenzo za elimu katika lugha ya asili.
- Kuboresha mahusiano na mawasiliano na majirani.
- Kuboresha utatuzi wa migogoro.
- Kuwezesha utetezi na upatikanaji wa taratibu za kisheria na za kiserikali katika lugha ya asili.
- Kuongeza upatikanaji wa taarifa kwenye mtandao kwa ajili ya elimu, biashara, na ushiriki wa kijamii, aidha katika lugha ya asili au lugha nyingine kadiri zana za tafsiri zinavyoendelea kuimarika.
- Kuwaletea wengine utambuzi wa lugha ya asili, utamaduni na hekima.
- Kupanua nafasi na mwonekano wa jamii za asili kimataifa.
- Kuwawezesha makundi yaliyotengwa au yaliyopuuzwa kudumisha au kufufua lugha yao licha ya kuzingirwa na makundi yaliyotawala.
- Kuhifadhi mifumo asili ya maarifa, utamaduni, historia, sanaa, tiba, hekima, maadili, na mtazamo wa dunia.